

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

Anwani ya Simu: "UCHUNGUZI"
Simu Nambari: 027- 2 750885
Fax No 027-2750889
e – mail:rbckilimanjro@pccb.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:



S.L.P. 1951,
MOSHI,
TANZANIA.

TAARIFA KWA UMMA

KILIMANJARO JUNI 4, 2020

**ALIYEKUWA MGANGA MKUU NA MFAMASIA ROMBO
WAFIKISHWA MAHAKAMANI KWA RUSHWA**

na

**MWAMUZI WA MPIRA WA MIGUU MOSHI AHUKUMIWA KIFUNGO
JELA KWA RUSHWA**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoani Kilimanjaro imewafikisha katika Mahakama ya Wilaya Rombo aliyekuwa Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, Dkt Christon Nkya na aliyekuwa mfamasia wa halmashauri hiyo Remig Massawe mnamo tarehe 2 juni, 2020.

Dkt Nkya ambaye ni mstaafu kwa sasa na Remig Massawe ambaye kwa sasa ni Mfamasia wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, wamefikishwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU Furahini Kibanga na kufunguliwa kesi ya Jinai "Corruption Case". Na. 1/2020 mbele ya hakimumu wa mahakama hiyo Mheshimiwa Regina Futakamba.

Wawili hao wanashtakiwa kwa makosa matatu; (i) Kughushi kinyume na kifungu cha 333, 335(a) na 337 vya Sheria ya Kanuni za Adhabu, (ii) Matumizi mabaya ya mamlaka kinyume na kifungu cha 31 na (iii) kutumia

nyaraka kwa lengo la kumdanganya mwajiri kinyume na kifungu cha 22, vyote vya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11/2007. Jumla ya fedha inayohusika ni shs 1,588,000.00.

Washtakiwa wote wako nje kwa dhamana baada ya kutimiza masharti yaliyowekwa na mahakama ya kuwa na wadhamini wawili wanaoaminika watakaotia saini bondi ya shs 1,000,000.00 kila mmoja.

NA KATIKA HATUA NYINGINE,

Mnamo tarehe 22 mei, 2020, Mahakama ya Mkoa wa Kilimanjaro ilimtia hatiani mshtakiwa **Safiel Elias Mjema**, aliyekuwa ni Mwamuzi wa mpira wa miguu, kutumikia kifungo cha mwaka mmoja jela au kulipa faini ya shilingi laki tano (500,000/=). Mtuhumiwa alishindwa kulipa faini hiyo na hivyo alipelekwa jela kutumikia kifungo cha mwaka mmoja jela.

Awali mtuhumiwa huyo alifikishwa mahakamani hapo akikabiliwa na kosa la kuomba na kupokea hongo kiasi cha shs laki moja na elfu ishirini (120,000/=) ili aweze kutoa upendeleo kwa timu ya "New Generation" iliyokuwa ikicheza na timu ya La Familia kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na. 11/2007.

TAKUKURU Mkoa wa Kilimanjaro, tunatoa Rai kwa wanamichezo kutojihusisha na vitendo vya rushwa kwa namna yoyote ile kwani vinadumaza maendeleo ya michezo na ustawi wa jamii yetu. Vilevile tunatoa Rai kwa wananchi wote kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa taarifa kwa ofisi yetu iliyo karibu au kupitia namba yetu ya dharura 113

Imetolewa na,

FIDELIS KALUNGURA

MKUU WA TAKUKURU (M)
KILIMANJARO